JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

TAARIFA YA MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE DESEMBA 2005 HADI DESEMBA, 2009

WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI
S.L.P 9152,
DAR ES SALAAM

FEBRUARI 2010

WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE DESEMBA, 2005 HADI DESEMBA, 2009

1.0 UTANGULIZI

Kulingana na Muundo wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara imepewa majukumu yafuatayo:-

(i) Kutayarisha, kurekebisha na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mipango na Mikakati ya kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi;
(ii) Kutayarisha, kurekebisha na kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu katika Sekta za Mifugo na Uvuvi;
(iii) Kufanya na kuimarisha utafiti wa mifugo na Uvuvi;
(iv) Kuimarisha huduma za ushauri za mifugo na uvuvi;
(v) Kudhibiti magonjwa ya mifugo na samaki pamoja na wadudu wanaoeneza magonjwa hayo;
(vi) Kudhibiti na kukagua ubora, usalama na viwango vya mazao ya mifugo na uvuvi pamoja na zana na pembejeo;
(vii) Kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza takwimu na taarifa muhimu za Sekta za Mifugo na Uvuvi;
(viii) Kutoa mafunzo kwa watumishi, wanafunzi watarajali, na wadau wengine wa Sekta za Mifugo na Uvuvi;
(ix) Kushirikisha Halmashauri za Wilaya, Taasisi za Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa, sekta binafsi, wadau mbalimbali pamoja na jamii za wafugaji na wavuvi katika ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo, uvuvi na mazingira;
(x) Kusimamia Bodi na Asasi zilizo chini ya Wizara;
(xi) Kukusanya maduhuli kutokana na vyanzo mbalimbali vya sekta; na
(xii) Kuendeleza rasilimali watu katika fani za mifugo na uvuvi.

Majukumu haya yanatekelezwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa CCM ya mwaka 2005, Dira na Dhima ya Wizara pamoja na mikakati mbalimbalii ya Kitaifa.

2.0 DIRA NA DHAMIRA

2.1 Dira

Kuhakikisha kuwa rasilimali za mifugo na uvuvi zinaendelezwa na kutunzwa katika mazingira endelevu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

2.2 Dhamira

Kuhamasisha, kuwezesha na kusimamia kukua kwa ufugaji wa kisasa na uvuvi endelevu; uzalishaji bora wa mifugo na uvuvi pamoja na mazao yake; na utoaji wa huduma bora kwa wadau wa sekta ili kuwa na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Dhamira hii itafanikiwa kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuzijengea uwezo wa kitaalamu na kitaaluma Serikali za Mitaa ili kutoa kwa ufanisi huduma bora kwa wafugaji na wavuvi;

(ii) Kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi katika kutoa huduma na kuzalisha mazao bora ya mifugo na uvuvi kwa ajili ya soko la ndani na nje; na

(iii) Kushughulikia mahitaji ya wafugaji, wavuvi pamoja na watumiaji wa mazao ya mifugo na uvuvi.

3.0 MAFANIKIO YA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

Katika kipindi cha miaka minne kuanzia Desemba, 2005 hadi Desemba, 2009, Wizara imetekeleza majukumu yake na mafanikio ya utekelezaji yameainishwa katika maeneo yafuatayo:

3.1 Sekta ya Mifugo

3.1.1 Kuongezeka kwa Uzalishaji wa Mazao ya Mifugo: Maziwa, Nyama na Mayai

Ili kuongeza uzalishaji wa maziwa pamoja na ulaji wake, Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusindika maziwa, uundwaji wa vikundi vya kukusanya na kusindika. Usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **56,580** kwa siku mwaka 2004/2005 hadi lita **88,940** mwaka 2008/2009 sawa na ongezeko la asilimia **57.2**. Aidha, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **bilioni 1.4** mwaka 2004/2006 hadi lita **bilioni 1.6** mwaka 2008/2009 sawa na ongezeko la lita milioni 200 (asilimia 13.8)**.**

Katika kipindi hicho, uzalishaji wa nyama uliongezeka kutoka tani **378,509** hadi tani **422,230**. Kati ya hizo tani **225,178** nyama ya ng'ombe, tani **82,884** za mbuzi na kondoo, tani **36,000** za nguruwe na tani **78,168** ni za nyama ya kuku.

Aidha, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka mayai **bilioni 1.8** hadi mayai **bilioni 2.8** mwaka 2008/2009 sawa na ongezeko la mayai **bilioni 1.0** (asilimia **55.6**). Ongezeko hili limetokana na mwitikio wa wafugaji kutumia chanjo stahimilifu ya joto ya kuzuia ugonjwa wa mdondo wa kuku. Chanjo hii imepunguza vifo vya kuku wa asili.

3.1.2 Kuimarisha Mashamba ya Uzalishaji Mitamba

Wizara imenunua jumla ya ng'ombe wazazi **570** na madume **10** kwa ajili ya mashamba ya kuzalisha mitamba ya Mabuki, Nangaramo, Sao Hill na Ngerengere ili kuimarisha uzalishaji. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali imesambaza jumla ya mitamba **24,549** na mbuzi wa maziwa **5,379** kupitia mpango Kopa Ng'ombe/Mbuzi, Lipa Ng'ombe/Mbuzi katika mikoa yote nchini katika kipindi cha mwaka 2004/2005 hadi 2008/09.

3.1.3 Kuimarisha Uhimilishaji

Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji kama njia ya haraka ya kuboresha mifugo yetu. Hadi sasa Wizara imeanzisha vituo vya uhimilishaji katika Kanda za Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Mashariki (Kibaha) na Kati (Dodoma). Aidha, imenunua mitambo minne ya kutengeneza hewa baridi ya Naitrojeni (Liquid Nitrogen) kwa ajili ya Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) Arusha na vituo vya Kanda vilivyoanzishwa. Vilevile, madume **10** bora ya mbegu ya aina Ayrshire (**4**), Friesian (**5**) na Simmental (**1**) kutoka Afrika ya Kusini yamenunuliwa kwa ajili ya kuimarisha huduma hiyo katika kituo cha NAIC Arusha. Katika kipindi hicho, NAIC imezalisha jumla ya dozi **252,985** za mbegu za ng'ombe (semen) na ng'ombe 2**21,183** wamehimilishwa. Uwezo wa kuzalisha mbegu bora umeongezeka kutoka dozi **50,000** hadi dozi **340,000** kwa mwaka na uzalishaji halisi wa mbegu umeongezeka kutoka dozi **37,832** hadi **74,000** na uhimilishaji kutoka ng'ombe **28,950** hadi ng'ombe **68,900**. Mafanikio haya yanatokana na kuimarishwa kwa Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji – NAIC .

3.1.4 Kuongezeka kwa Mauzo ya Mifugo na Mazao yake

Jumla ya ng'ombe **2,496,829**, mbuzi **2,014,353** na kondoo **362,154** wenye thamani ya shilingi **bilioni 703.9** waliuzwa minadani. Aidha, jumla ya ng'ombe **13,042** na mbuzi **13,714** wenye thamani ya shilingi **bilioni 7.9** waliuzwa nje ya nchi, zikiwemo Comoro, Kenya, Burundi na Falme za Kiarabu. Vilevile, kiasi cha **tani 674.0** za nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo zenye thamani ya shilingi **bilioni 2.1** zimeuzwa nje ya nchi zikiwemo nchi za Oman, Saudi Arabia, Misri, Kuwait, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Comoro.

Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi unaendelea kutekelezwa katika Halmashauri **55** za mikoa **13** kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (LDF). Jumla ya vipande vya ngozi **milioni 7.12** za ng'ombe, **milioni 7.5** za mbuzi na **milioni 4.42** za kondoo vilizalishwa na kuuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa shilingi **bilioni 58.0**

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI pamoja na chama cha wadau wa ngozi nchini (Leather Association of Tanzania - LAT) Mkakati wa kufufua na kuendeleza Sekta ya Ngozi na Viwanda unaotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo. Jumla ya wataalam **160** na wadau wengine wa ngozi kutoka sekta binafsi **1,680** wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji, ukusanyaji na uhifadhi bora wa zao la ngozi katika Halmashauri **55**.

Vilevile, ili kuimarisha biashara ya mifugo na upatikanaji wa soko la ndani na nje, Wizara imeendelea kuhamasisha wadau wa mifugo kuunda vyama vyao. Katika kipindi hicho, Chama cha Wafanyabiashara wa Mifugo na Nyama Kitaifa (Tanzania Livestock and Meat Traders Association (TALIMETA) kilianzishwa. Aidha, Bodi za Nyama na Maziwa zilianzishwa kwa lengo la kuimarisha na kudhibiti uzalishaji wa nyama na maziwa nchini.

3.1.5 Kuimarisha Miundombinu ya Masoko ya Mifugo

Wizara imekarabati minada ya upili na mpakani katika maeneo mbalimbali nchini. Minada hiyo ni Pugu (Ilala), Lumecha (Songea), Meserani (Monduli), Igunga (Igunga), Kizota (Dodoma), Ipuli (Tabora Manispaa), Mhunze (Kishapu), Buhigwe (Kasulu), Kasesya (Sumbawanga) na Mbuyuni (Chunya) na kujenga minada ya Nyamatara (Misungwi) na Buzirayombo (Chato).

Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya mifugo imeendelea kuboresha mfumo wa utoaji wa taarifa za masoko ya mifugo (Livestock Information Network Knowledge System - LINKS) katika minada **45** ambayo hutoa taarifa za bei na aina ya mifugo inayouzwa pamoja na madaraja kwa kutumia ujumbe wa simu za mikononi (0787 441 555). Taarifa za masoko zinapatikana katika mtandao wa http://www.lmistz.net na kupitia tovuti ya Wizara http://www.mifugo.go.tz.

3.1.6 Kuimarisha Mfumo wa Kutambua, Kusajili na Kufuatilia Mifugo na Mazao yake

Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo unajumuisha kutambua mifugo kwa vitambulisho vya kudumu, kusajili mifugo iliyotambuliwa katika rejesta na kuwepo na taratibu za kusimamia na kuongoza matukio ya kuhamisha mifugo, ulishaji vyakula na matibabu. Mfumo huu unaendelea kuimarishwa ambapo hadi sasa mashamba ya mifugo **26** yenye jumla ya ngo'mbe **42,902,** mbuzi **3,793**, kondoo **1,134** na nguruwe **574** yametambuliwa kwa kusajiliwa kitaifa. Aidha, wafugaji wa asili **1,399** wenye jumla ya ng'ombe **133,321**, mbuzi **10,739**, kondoo **7,439**, kuku **12,392**, punda **67** wamesajiliwa kitaifa katika rejesta za vijijini. Pia, ng'ombe **124,552** wametambuliwa kwa chapa ya namba ya kitaifa inayoonyesha nchi (TZ), halmashauri (code ya jina) na kijiji (namba) inayokuwa pekee kwa kijiji nchi nzima. Kosaafu asili tisa (**9)** za ngo'mbe, tano (**5)** za mbuzi, moja (**1)** ya kondoo na tatu (**3)** za kuku zilitambuliwa na kusajiliwa.

Nakala **2,332** za rejesta za kusajili wafugaji na mifugo katika vijiji **2,332** vya wilaya **133** kwa ajili ya majaribio zimesambazwa. Aidha, vifaa vya chapa za moto **563** za utambuzi wa ngo'mbe kitaifa zilisambazwa katika Halmashauri **133** kwa majaribio. Pia, Maafisa Mifugo **290**, watendaji kata **5**, madiwani **30**, viongozi wa Halmashauri na mkoa (DED, DALDO RAS,RLA) **30**, wafugaji **1,137** na wafanyabiashara ya mifugo **25** kutoka katika Halmashauri zote na mikoa **21** walipata mafunzo ya usajili na utambuzi. Vilevile, nakala **500** za Jarida la Kitalaam la kuhamasisha wadau juu ya Utambuzi, Usajili na ufuatiliaji mifugo zilichapishwa na kusambazwa. Mtandao wa Komputa wa kutunza takwimu za usajili na utambuzi kitaifa umejengwa Makao Makuu ya Wizara. Utekelezaji wa mfumo huu umechangia kupunguza uhamaji holela wa mifugo kutoka sehemu moja ya nchi na kutoka nje ya nchi. Hata hivyo kumekuwepo na changamoto ya kupunguza udanganyifu wa mifugo inayopewa kitambulisho cha kitaifa ambao utadhibitiwa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo itapapokuwa imetungwa na Bunge, Rais kuridhia na kuanza kutekelezwa. Rasimu ya Muswada wa Sheria hii imeendaliwa.

Kutokana na juhudi za Tanzania katika kuanzaisha Mfumo huu imechaguliwa kuwa Mwenyeketi wa Kikosi Kazi cha Utambuzi na Ufuatiliaji Mifugo (Regional task Force on Livestock Identification & Traceability Systems for Eastern Africa) kwa Nchi **7** za Afrika Mashariki na Kati (Burundi, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan, Tanzania na Uganda).

Sambamba na Utambuzi na Usajili wa Mifugo, Ustawi wa Wanyama unaolenga kuwajali wanyama katika nyanja zote wanazotumiwa na binadamu kuzingatia wasipewe mateso na maumivu yanayoweza kuepukika Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na 19 ya Mwaka 2008 imetungwa na Kanuni zake nne zimeandaliwa. Utekelezaji wa Sheria hii na Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji Mifugo utachangia kuongeza nafasi ya ushindani katika soko la kimataifa kwa bidhaa/mazao ya mifugoinayozalishwa nchini.

3.1.7 Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)

Jukumu kubwa la NARCO ni kuzalisha, kunenepesha na kuuza mifugo kwa ajili ya nyama na kutoa huduma za ushauri kwa wafugaji wanaozunguka ranchi hizo. Kampuni imeendelea kuzalisha mifugo ya nyama katika ranchi zake **10** za mfano za Kikulula, Mabale, Kagoma, Misenyi, Kongwa, Mzeri, Ruvu, Mkata, Kalambo na West Kilimanjaro zenye eneo la hekta **230,284** na inao jumla ya ng'ombe **41,000**. Katika kipindi hiki Kampuni imeuza ng'ombe **36,331** wenye thamani ya shilingi **bilioni 9.0.**

Ili kuimarisha biashara ya nyama na mazao yake Serikali ilikubali kuuza asilimia **51** ya thamani ya mali za machinjio ya Dodoma kwa Kampuni ya National Investment Company Limited (NICOL) na kubakiza asilimia 49 chini ya NARCO. NARCO na NICOL zimeanzisha kampuni iitwayo *Tanzania Meat Company Limited* inayoendesha machinjio hiyo.

Aidha, Serikali imeiwezesha NARCO kuanza ujenzi wa machinjio kubwa na ya kisasa katika eneo la ranchi ya Ruvu mkoa wa Pwani. Itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **800** na mbuzi/kondoo **400** kwa siku.

3.1.8 Kuhamasisha Sekta Binafsi Kuwekeza katika Viwanda vya Kusindika Nyama na Maziwa

Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya kusindika nyama na maziwa. Ujenzi wa viwanda vya Sumbawanga Agricultural and Animal Feeds Industries (SAAFI) na Tanzania Pride Meat cha Morogoro umekamilika na viwanda hivyo vimeanza kufanya kazi. Kiwanda cha SAAFI kina uwezo wa kuchinja ng'ombe **150** kwa siku na Kiwanda cha Tanzania Pride Meat cha Morogoro kina uwezo wa kuchinja ng'ombe **200** na kuku **16,000** kwa siku.

Aidha, kiwanda cha Tanga Dairy kimepata mwekezaji mpya (Tanga Fresh Ltd) na kimeendelea na usindikaji wa maziwa. Kampuni ya New Musoma Dairy imeanza tena usindikaji wa maziwa na kiwanda cha Mara Milk kimeagiza mtambo wa kusindika maziwa yenye uwezo wa kukaa muda mrefu zaidi bila kuharibika (kiwango cha UHT).

3.1.9 Kuboresha Upatikanaji Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo

(i) Ujenzi wa Mabwawa na Malambo

Ili kukabiliana na uhaba wa maji kwa ajili ya mifugo, Wizara imekarabati na kujenga malambo **20** na mabwawa **2**. Aidha, kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) jumla ya malambo **217** yamejengwa katika maeneo mbalimbali. Pia, kupitia Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (PADEP) jumla ya malambo **193** yamekarabatiwa na kujengwa ambapo visima virefu **39** vimechimbwa. Vilevile, jumla ya malambo **107** yamejengwa na kukarabatiwa kupitia mradi wa DASIP (**60)** na TASAF (**47)**.

(ii) Utengaji Maeneo ya Malisho

Kati ya hekta **milioni 60** zinazofaa kwa ufugaji asilimia **40** ya eneo hilo (sawa na hekta **milioni 24**) zinakaliwa kwa wingi na ndorobo, hivyo kuacha asilimia **60** (sawa na hekta **milioni 36**) zinafaa kwa ufugaji. Hadi sasa jumla ya hekta **1,391,109.41** sawa na asilimia **3.8** ya eneo lote linalofaa kwa ufugaji limetengwa katika vijiji **240** vya Halmashauri za Wilaya **31** za mikoa **13** kwa ajili ya ufugaji. Ili kuendelea kutenga maeneo ya wafugaji, Halmashauri zinahimizwa kuendelea kuainisha, kutenga na kumilikisha maeneo kwa wafugaji na kuhakikisha yanaendelezwa. Aidha, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Asasi zisizo za Serikali inatekeleza programu ya kuelimisha wafugaji wa asili kuhusu Sheria za Ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Vilevile, jumla ya wafugaji **259** wa mikoa ya Kanda ya Ziwa (**30**) na Lindi (**229**) wamepatiwa mafunzo kuhusu matumizi bora ya ardhi. Aidha, mapendekezo ya kutunga Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo (Grazingland and Animal Feed Resources Act) imewasilishwa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kujadiliwa kwa hatua zaidi.

Mafunzo yalitolewa kwa wataalam kuhusu matumizi bora ya ardhi katika Chuo cha Mafunzo ya Mifugo Morogoro katika Halmashauri za wilaya **18** za Monduli, Ngorongoro, Kilosa, Chamwino, Lindi Vijijini, Kilwa, Nachingwea, Simanjiro, Chunya, Mvomero, Bagamoyo, Kisarawe, Nkasi, Namtumbo, Manyoni, Bukombe, Kishapu, Urambo na Handeni.

Aidha, wafugaji **60** na wataalam **43** kutoka Halmashauri za Bagamoyo, Bukombe, Handeni, Kishapu, Mvomero, Namtumbo, Nkasi, Kilwa, Kahama, Kishapu, Maswa, Urambo, Dodoma Vijijini, Igunga, Kondoa, Kongwa, Manyoni, Mpwapwa, Nzega na Singida Vijijini walipata mafunzo kuhusu uandaaji wa mipango ya matumizi endelevu ya ardhi ya mifugo.

(iii) Kuimarisha Mashamba ya Malisho na Kuanzisha Mashamba Mapya

Wizara imeendelea kuimarisha mashamba ya uzalishaji mbegu bora za malisho ya Vikuge (Kibaha) na Langwira (Mbarali) na mashamba mapya ya Mabuki, (Misungwi) Buhuri (Tanga) Kizota (Dodoma Manispaa), Kongwa, Mivumoni (Muheza) na Sao Hill (Mufindi). Mashamba hayo yamezalisha jumla ya tani **84.4** za mbegu aina mbalimbali na marobota **929,680** ya hei na kuyasambaza kwa wafugaji.

Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa malisho bora. Kutokana na uhamasishaji huo, kumekuwepo na ongezeko la wazalishaji binafsi wa malisho bora kutoka wawekezaji **6** mwaka 2006 hadi **40** mwaka 2008, ambapo jumla ya tani **18.5** za mbegu bora na marobota **509,980** ya hei yamezalishwa.

(iv) Uzalishaji wa Vyakula vya Mifugo kutoka katika Sekta Binafsi

Kuanzia mwaka 2006 hadi 2008 jumla ya tani **milioni 1.2** za vyakula vya mifugo zimezalishwa na sekta binafsi. Wizara ilitoa mafunzo kwa wakaguzi **20** wa vyakula vya mifugo kutoka Halmashauri **15** za Dodoma, Ilala, Ilemela, Iringa, Kibaha, Kinondoni, Mbeya, Morogoro, Moshi, Muheza, Nyamagana, Sumbawanga, Tabora, Tanga na Temeke. Wakaguzi hawa watashauri na kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo.

3.1.10 Kuimarisha Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo

(i) Uchunguzi wa Mwenendo wa Magonjwa ya Mifugo

Mfumo wa utoaji tahadhari mapema kuhusu matukio ya magonjwa uliimarishwa. Vijitabu **2,000** vya taratibu za ufuatiliaji (Standard Operation Procedures) na utoaji taarifa za magonjwa ya mlipuko (TADs) na vijitabu **2,000** vyenye maelekezo mafupi kuhusu magonjwa (extension messages na disease fact sheets) vilisambazwa katika Halmashauri zote nchini. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wataalamu wa VICs na Makao Makuu ili kuwawezesha kutoa takwimu na taarifa za magonjwa ya mifugo kwa kutumia mfumo wa TADinfo ulioanzishwa na Shirika la Chakula Duniani (FAO).

Wizara ikishirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), imeanzisha matumizi ya tekinolojia ya kalamu ya "digital" katika wilaya za Dodoma, Hai, Ngorongoro, Monduli, Same, Misenyi, Kyela, Tarime na Serengeti kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa za afya ya mifugo. Tekinolojia hii imewezesha kuongezeka upatikanaji wa takwimu kutoka asilimia **40** hadi kufikia asilimia **70**.

Kutokana na kuimarika kwa mifumo ya ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya mlipuko, Ugonjwa wa Sotoka umetokomezwa na nchi yetu kutambuliwa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) kuwa huru na virusi vya ugonjwa wa Sotoka kuanzia mwaka 2007.Tathmini ya ufanisi wa Huduma za Mifugo Nchini ilifanyika mwaka 2009 na wataalamu kutoka Shirika la Afya ya Wanyama Ulimwenguni (OIE) kwa kushirikiana na wataalamu wa Wizara ambapo mpango mkakati wa kuboresha huduma hizo unaandaliwa.

Mnamo mwezi Januari mwaka 2008, ugonjwa wa "sotoka ya mbuzi na kondoo" (Peste des Petits Ruminants - PPR), uliingia nchini kwa mara ya kwanza ukitokea nchi jirani. Ugonjwa huu uliathiri mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara, ambako inakisiwa kwamba, jumla ya mbuzi **1,730,268** na kondoo **1,051,986** waliathirika. Kati ya hao, mbuzi **96,549**, na kondoo **58,701**, walikufa kutokana na ugonjwa huu. Katika jitihada za Serikali kudhibiti ugonjwa huu, Wizara ilishiriakiana na shirika lisilo la kiserikali la VetAid, na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kuchanja wanyama waliokuwa katika hatari ya kuambukizwa. Jumla ya mbuzi na kondoo **1,820,276** walichanjwa kwenye mikoa iliyoathirika. Aidha, uchunguzi wa Sotoka ya mbuzi na kondoo katika Kanda za Kaskazini na Ziwa zilifanyika na sampuli **3,882** za damu zilichukuliwa na kufanyiwa uchunguzi.

Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) inaendelea na mpango wa kuchanja mbuzi na kondoo **milioni 3.5** katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mwanza, Shinyanga, Singida na Tanga.

(ii) Udhibiti wa Magonjwa ya mifugo

Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP)

Ugonjwa huu umeendelea kudhibitiwa kwa mpango wa "Rollback Plan". Kiasi cha chanjo dozi **milioni 13.4** zilinunuliwa na idadi ya ng'ombe **milioni 11.1** kuchanjwa katika mikoa ya Tabora, Kagera, Kigoma, Shinyanga, Singida, Iringa, Mbeya na Rukwa. Ugonjwa huu umedhibitiwa katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Rukwa ambapo tangu mwaka 2007 hapajatokea mlipuko.

Ugonjwa wa Miguu na Midomo

Mpango wa kitaifa wa kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD umeandaliwa. Ufuatiliaji wa ugonjwa huu ulifanyika katika kanda ya Nyanda za juu kusini ambapo iligundulika FMD virus type A katika mikoa ya Mbeya na Iringa.

Mpango wa Kudhibiti Mafua Makali ya Ndege (HPAI-H5N1)

Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege bado ni tishio duniani na unaendelea kuenea. Kwa mujibu wa taarifa kutoka Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) hadi kufikia machi 2009 nchi **62** zilikuwa zimeambukizwa ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege, kati ya nchi hizo, **11** zipo katika bara la Afrika nazo ni Nigeria, Misri, Niger, Cameroon, Burkina- Faso, Sudan, Cote d'Ivore, Djibouti, Ghana, Benin na Togo. Tokea ugonjwa uanze 2003 hadi sasa, zaidi ya watu **467** wameugua na kati yao watu **282** wameshapoteza maisha kwa sababu ugonjwa huo katika nchi **15** zilizotoa

taarifa ya matukio ya ugonjwa kwa binadamu. Jumla ya sampuli **22,300** za ndege pori, kuku na bata zilikusanywa na kuthibitishwa kutokuwepo kwa ugonjwa huu nchini.

Mkakati wa Kitaifa wa kudhibiti tishio la ugonjwa huu umeandaliwa na kuzindiliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 28 Aprili 2008. Utekelezaji wa mpango mkakati huo ulianza chini ya Ufadhili wa UNICEF, FAO, WHO Umoja wa Nchi za Afrika (AU) na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) ili kuchukua tahadhari. Utekelezaji wa mkakati huo umefanyika kwa kutoa elimu kwa umma, mafunzo kwa wataalam na waalimu za shule za msingi pamoja na ununuzi wa vifaa vya kinga na vya maabara.

Jumla ya vipindi **4** runinga vilitayarishwa na kurushwa hewani. Aidha, vipeperushi **1,020,000** na mabango **1,000,000** vilichapishwa na kusambazwa. Nakala **500** za mpango mkakati na kalenda **500** zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Aidha, vijitabu **2,000** vya kufundisha wataalam na nakala **5,000** za vijitabu/vijarida na mabango kwa ajili ya wanafunzi mashuleni zilisambazwa. Mabango **10,000** kwa ajili ya wafanya biashara wa kuku na vituo vya ukaguzi wa Mifugo vya mipakani vilichapishwa na kusambazwa. Mafunzo kwa Maafisa Mifugo, Madaktari wa Afya, Maafisa Maliasili na yalifanyika ambapo washiriki **1,630** walifundishwa. Mafunzo kwa wadau wengine wakiwemo madiwani, waandishi wa habari na mashirika yasiyo ya kiserikali yalifanyika; jumla ya washiriki **250** walifundhishwa katika mikoa ya kanda ya Ziwa, Magharibi, Kusini na Mashariki.

Maabara zetu kwa kushirikiana na Wahisani, Marekani kupitia shirika la USAID wametoa fedha kiasi cha dola za kimarekani 700,000 kwa ajili ya kuzijengea uwezo Maabara Kuu ya Mifugo Temeke (CVL), Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) kutambua na kufuatilia ugonjwa huu.

(iii) Magonjwa ya Kuambukiza Binadamu

Ugonjwa wa Bonde la Ufa

Mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ulitokea hapa nchini mwezi Januari mwaka 2007 na kudhibitiwa ilipofika Juni 2007. Mafanikio haya yalitokana na uchanjaji uliofanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Jumla ya dozi **milioni 5.5** zilinunuliwa na mifugo ipatayo **milioni 4.9** ilichanjwa katika Halmashauri **52**, mashamba ya ng'ombe wa maziwa, Utafiti na Ranchi za Taifa. Tathmini ya kiuchumi ya kijamii ya mlipuko wa Homa ya Bonde la Ufa

ilifanyika ilionyesha kwamba Mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa uliotokea mwaka 2007 ulileta athari kubwa za kiuchumi na kijamii kuliko vipindi vyote vya nyuma. Hamasa na elimu kwa wananchi ilitolewa ambapo vipeperushi **1,000** viligawiwa kwa wananchi. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa kudhibiti ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa iwapo utatokea.

Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa

Mpango Mkakati wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa umeandaliwa. Mpango mkakati huo umeanza kutekelezwa kwa kuchanja mbwa na paka. Jumla ya dozi **342,988** za chanjo ya Kichaa cha Mbwa zilinunuliwa na kusambazwa kwa wilaya **30** ambapo jumla ya mbwa na paka **285,567** walichanjwa. Jumla ya vipeperushi **5,200** vimesambazwa kwa wananchi.

Aidha, serikali inatekeleza mradi wa kudhibiti kichaa cha mbwa unaofadhiliwa na Taasisi ya Bill na Belinda Gates. Mradi huu ni wa miaka miaka mitano (2009 hadi 2013) na umepatiwa jumla ya **Dola za Kimarekani milioni 3.9** na utatekelezwa katika wilaya **24** kwenye mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara na mbwa wapatao **400,000** watachanjwa. Kitengo kilishiriki kwenye maonyesho ya nanenane ambapo vilisambazwa. Aidha, vipindi vinne vya redio na kimoja cha runinga viliandaliwa na kurushwa kwa ajili ya kuelimisha umma.

Ugonjwa *wa Kutupa Mimba (Brucellosis) na Kifua Kikuu cha Ng'ombe (Bovine Tuberculosis)*

Uchunguzi wa magonjwa haya hufanyika katika Vituo vya uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo (Veterinary Investigation centres) vya Kanda ambapo hupata fedha kutoka Wizarani. Katika kipindi hiki jumla ya ng'ombe **3,728** na mbuzi **340** walifanyiwa uchunguzi wa Ugonjwa wa Kutupa Mimba ambapo ng'ombe **176** waligundulika kuwa na ugonjwa na walichinjwa. Aidha, jumla ya dozi **5,000** (S19) zilinunuliwa na Taasisi binafsi na jumla ya ng'ombe **3,500** walichanjwa. Jumla ya ng'ombe **147** walifanyiwa uchunguzi wa Ugonjwa wa Kifua Kikuu na **10** waligundulika kuwa na Ugonjwa.

(iv) Magonjwa yaletwayo na Kupe na Ndorobo

Serikali ya awamu ya nne imetoa jumla ya shilingi **bilioni 12.5** kama ruzuku kwa ajili ya ununuzi wa dawa za kuogesha mifugo kwa mikoa yote Tanzania Bara. Lengo la fedha hiyo ni kuwawezesha wafugaji kuzinunua na kuogesha mifugo yao na hivyo kupunguza hasara ziletwazo na kupe na magonjwa wayaenezayo ambazo zinakadiriwa kuwa takribani shilingi **bilioni 70** kwa kila

mwaka. Wafugaji huuziwa dawa hizo kwa asilimia **60** ya bei halisi na asilimia **40** iliyobaki inalipwa na Serikali kama ruzuku. Jumla ya lita **827,616** za dawa za kuogesha mifugo zilinunuliwa nje ya nchi na nyingine kutengenezwa hapa nchini na kusambazwa katika mikoa yote.

Kupitia Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Wilayani (DADPs) na Sekta binafsi, jumla ya majosho **684** yamekarabatiwa na **205** kujengwa kwa ajili ya kuogesha mifugo na kufanya majosho yaliyo katika hali nzuri ya kufanya kazi nchini kuwa **1,548** kati ya majosho **2,347** yaliyopo nchini. Aidha, katika kipindi hivho, ng'ombe **295,556** walipatiwa chanjo ya kinga dhidi ya ugonjwa hatari wa Ndigana Kali.

Halmashauri za mikoa ya Singida, Mtwara, Ruvuma, Pwani, Tabora, Manyara, Morogoro, Iringa na Mbeya ziliripoti kuwepo kwa matatizo ya mbung'o na ndorobo. Maafisa Ndorobo wasaidizi **15** kutoka halmashauri hizo walipatiwa mafunzo ya kudhibiti mbung'o na ndorobo. Aidha, mafunzo ya kudhibiti mbung'o kwa kutumia tekinolojia shirikishi yalitolewa kwa wafugaji wa mkoa wa Lindi (Lindi Vijijini -wafugaji **168** na Kilwa -wafugaji **61**). Jumla ya vijiji **22** vilishiriki katika mafunzo hayo, vijiji **14** vya wilaya ya Lindi Vijijini na **8** vya wilaya ya Kilwa. Aidha, wataalamu **16** wa Lindi vijijini na 5 wa wilaya ya Kilwa walishiriki. Pia, uchunguzi wa mtawanyiko wa mbung'o ulifanyika katika mikoa ya Kagera, Mwanza na Tabora na ramani mpya ya mikoa hiyo **mitatu** ilichorwa ili kuweza kutumika katika mkakati wa kutokomeza mbung'o.

Matukio ya ugonjwa wa Nagana katika mifugo yaliendelea kupungua kutoka **7,007** kwa mwaka 2005 na kufikia wastani wa **1,657** kwa mwaka 2009. Mafanikio haya yalitokana na matumizi ya dawa za ruzuku ya serikali aina ya pareto (synthetic pyrethroids) ambazo zinaua kupe na mbung'o na kwa sasa zinasambazwa kwa wafugaji wengi.

(v) Utekelezaji wa Mradi wa Jumuiya ya Kusini mwa Afrika wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko

Mradi wa Jumuiya ya kusini mwa Afrika wa kuimarisha Taasisi zinazodhibiti magonjwa ya mlipuko ya mifugo unatekelezwa katika nchi ya Tanzania, Angola, Zambia, Malawi na Msumbiji. Madhumuni ya mradi ni

(i) kuimarisha uwezo wa nchi katika kuchunguza, kutambua na kudhibiti magonjwa ya mlipuko;

(ii) kuimarisha huduma za mifugo hasa maabara na vitengo vya epidemiologia kwa kuvipatia vifaa na kutoa mafunzo wataalamu ili vifikie viwango vinavyopendekezwa na OIE;

(iii) kufanya tafiti za athari za kichumi na kijamii zinazosababishwa na magonjwa ya mlipuko ya mifugo; na
(iv) kuboresha mahusiano ya Taasisi na nchi zinazotekeleza mradi.

Tanzania ilipatiwa Dola za kimarekani **5,888,089** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kupitia Jumuia ya kusini mwa Afrika (SADC) ili kutekeleza mradi huu kwa kipindi cha miaka mitano (2007 – 2012). Utekelezaji wa mradi tangu uanze ni kama ifuatavyo:-

(i) Ununuzi wa vifaa vya ofisi (Computer **10**, laptop **3**, printer **12** na vifaa vyake) kwa ajili ya matumizi ya Vituo vya Uchunguzi wa magonjwa ya mifugo (VICs), kitengo cha Epidemilojia na ofisi ya Mratibu wa mradi.
(ii) Ununuzi wa vifaa vya maabara (reagents na consumables) – Rinderpest kit kwa ajili ya kupima sampuli **5,000** na kemikali kwa ajili ya kazi mbali mbali za Maabara Kuu ya Mifugo vimenunuliwa.
(iii) Ununuzi wa magari na pikipiki kwa ajili ya mradi – Wizara imesaini mkataba baina yake na City Motors (T) Ltd kwa ajili ya kununua pikipiki **10**. Aidha, Wizara imesaini mkataba na DT Dobie (T) Ltd kwa ajili ya ununuzi wa magari **tisa** (**9**).
(iv) Kujenga uwezo wa wataalamu na wadau – Wataalam na wadau wa mifugo **134** walihudhuria warsha na semina mbali mbali zilizoandaliwa na mradi. Vilevile watumishi wapatao **87** walihudhuria mafunzo mbali mbali kuhusu sekta ya mifugo ndani na nje ya nchi.

3.1.11 Kuimarisha Baraza la Veterinari

Baraza la Veterinari limesimamia na kufuatilia maadili ya watoa huduma za afya ya mifugo. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kusajili na kuandikisha watalaam na vituo kama ifuatavyo:

- Kusajili madaktari wa mifugo **107** na kufanya idadi ya madaktari wa mifugo waliosajiliwa kufikia **601,** ambapo 13 kati yao wamefariki.
- Kuandikisha na kuorodhesha Wataalam Wasaidizi **769** na kufanya idadi kufikia **1005.**
- Kusajili vituo **82** vya kutoa huduma za mifugo na kufanya idadi ya vituo vilivyosajiliwa kufikia **296.** Aidha, vituo 4 katika mkoa wa Dar es Salaam vilifungwa kwa kutozingatia viwango vilivyowekwa. Vituo hivyo vilifanya marebisho na kufikia viwango na kufunguliwa baada ya wiki tatu.

- Kuelimisha wakaguzi wa maadili wa wilaya **136** na Maafisa washauri wa mifugo wa mikoa **26** juu ya maeneo ya kushirikisha sekta binafsi katika utoaji huduma bora za mifugo kupitia semina za kimafunzo zilizofanyika kikanda.
- Kuandaa na kuhamasisha kanuni **14** za kusimamia mitaala ya kufundishia wataalam, ukaguzi wa huduma, maadili ya madaktari na wataalam wasaidizi wa mifugo na kuchapisha na kusambaza nakala 8**,000** za sheria, kanuni na miongozo.
- Kuteua wakaguzi wa maadili **153** (**2** Madaktari – Sekta Binafsi) chini ya sheria ya Veterinari Na. 16 ya mwaka 2003. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri, Baruza limefuatilia na kufanya ukaguzi wa watoa huduma katika Halmashauri 123 pamoja na vituo **8** vimekaguliwa. Wataalam 6 walipata maonyo makali na 1 amepelekwa mahakamani.
- Kuboresha mazingira ya wataalamu wa huduma za mifugo ili kusogeza huduma hizo kwa walengwa kwa kuhamasisha kuanzisha vituo vya afya ya mifugo katika vyuo vya mafunzo 2, maeneo yenye mifugo kwenye halmashauri 109 na mashamba makubwa ya mifugo.
- Kuboresha programme ya computer 1 inayowezesha kutunza kumbukumbu za usajili, kuchapisha vyeti na kuwa na mawasiliano na wadau wote nchini kupitia mtandao.
- Kuchangia katika kuboresha viwango vya taaluma kikanda na kimataifa kwa kushiriki kuweka mitaala kwa kuandaa mkutano wa kanda (OIE/SADC) uliofanyika Arusha, na kimataifa (OIE) ulifanyika Ufaransa.
- Kuwezesha vyama 2 vya wataalamu (Tanzania Veterinary Association na Tanzania Veterinary Paraprofessional Association) kufanya mikutano yao ya kitaifa na kikanda.
- Kuhamasisha ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutoa huduma za afya ya mifugo kwenye Halmashauri za mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, DSM, Morogoro, Dodoma na Singida.

3.1.12 Kuimarisha Huduma za Utafiti

(i) Tafiti za Mifugo na Malisho

- Uchanganyaji wa damu ya ng'ombe wa kigeni na wa asili (*cross-breeding*) umeongeza kiwango cha kuzaa kutoka asilimia **40** hadi **55** na muda kati ya mzao mmoja na mwingine umeshuka kutoka miezi **24** hadi **20**. Aidha, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka wastani wa lita **1** - **2** kwa siku kwa ng'ombe wa asili hadi wastani wa lita **6** - **8** kwa siku kwa ng'ombe chotara.

- Uchambuzi wa kosaafu (breed characterazation) za mifugo ya asili ng'ombe aina ya Iringa Red, Singida White, Ufipa na Ankole; na mbuzi aina ya Gogo White, Newala, Pare White, Sonjo Red na Ujiji na kwa kuku wa asili aina ya Kuchi, Bukini, Kinyavu/Sasamala, Kiduchu/Kikwekwe, Ntewa, Kisunzu na Kishingo kwa lengo la kutambua sifa walizo nazo na kuwafanyia tathmini vituoni.

- Utafiti wa uzalishaji wa nyama kwa kuchagua (selection) na kuchanganya damu za kigeni na zile za asili umeongeza uzito wa ng'ombe kutoka wastani wa kilo 250 hadi kufikia kilo 400 katika umri wa miaka minne kwa mazingira ya wafugaji wa Wilaya za Bagamoyo, Handeni, Longido, Monduli na Mpwapwa.

- Utafiti wa mbuzi wa asili kwa kuboresha lishe, mabanda na afya umeongeza uzito kutoka wastani wa kilo 25 hadi 30 katika umri wa miaka miwili. Vilevile, vifo vya watoto wa mbuzi vimepungua kutoka asilimia 50 hadi 15. Aidha, jumla ya mbuzi bora 300 wamesambazwa katika wilaya za Iramba, Manyoni, Dodoma (Manispaa), Chamwino, Mpwapwa, Kondoa, Kongwa, Singida Vijijini, Simanjiro, Kibaha, Shinyanga, Kishapu, Mtwara, Kinondoni, Bahi, Maswa na Ngorongoro.

- Ndama 723 wa ng'ombe aina ya Mpwapwa walizaliwa katika Kituo cha Mpwapwa. Madume 293 yamesambazwa vijijini katika wilaya za Iramba (40), Mpwapwa (25), Kongwa (8), Chunya (40), Manyoni (70), Igunga (20), Shinyanga (10), Mbeya (8), Kiteto (12), Arusha (8), Bahi (50) na Chamwino (2) ili kuinua kiwango cha uzalishaji wa ng'ombe wa asili. Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka wastani wa lita 1 – 2 kwa siku hadi lita 3 – 4 kwa siku,uzito wa kuzaliwa (ndama) kutoka kilo 10 – 15 hadi kilo 15 – 20, umri wa kupevuka (madume na majike) umepungua kutoka miaka 3 - 4 hadi kufikia miaka 2 – 3 kwa ng'ombe wa asili na chotara.

- Utafiti unaolenga kuboresha nguruwe wa asili umeendelea kufanyika katika kaya 125 za Wilaya ya Sumbawanga Vijijini, Rungwe na Mbozi. Aidha, tathmini ya tiba za asili kwa kutumia Utupa kutibu ugonjwa wa ukurutu na usambazaji wa nguruwe bora 130 umefanyika katika wilaya za Mpwapwa na Kongwa.

- Utafiti unaonyesha kuwa kuku wa asili anapopewa chakula cha ziada baada ya kujitafutia chakula wao wenyewe; utagaji wa mayai unaongezeka kutoka wastani wa mayai 10 hadi kufikia kati ya mayai 18 hadi 25 kwa mtago. Ukuaji wa vifaranga unaongezeka kutoka wastani wa gramu kati ya 3 na 5

hadi kufikia wastani wa gramu 8 na 10 kwa siku. Kiwango hiki cha ukuaji kinaonyesha kuwa kuku anaweza kufikia kati ya kilo 1½ hadi kilo 2 kwa kipindi cha miezi 6 tu. Aidha, kuachisha makinda/viranga ndani ya wiki 4 kunaongeza idadi ya mitago kutoka wastani 2 - 3 kwa mwaka hadi wastani wa mitago 6 - 8 kwa kolowa kwa mwaka na hivyo kuongeza idadi ya mayai kutoka wastani wa mayai 40 - 60 hadi 90 - 120 kwa kolowa kwa mwaka.

- Kilogramu 8,215 za mbegu za *Chloris gayana* na *Cenchrus ciliaris* na kilogramu 906 za aina mbalimbali za mikunde zikiwemo *Centrosema pubescens, Macroptilium atropurpureum, Lablab purpureus* na *Clitoria ternatea* zilizalishwa katika vituo vya Mpwapwa, Mabuki, Tanga na Uyole. Kilogramu 2,097 za nyasi na kilogramu 154.5 za mikunde ziliuzwa kwa ajili ya kuendeleza malisho katika wilaya mbalimbali zikiwemo Mpwapwa, Nkasi, Mbarali, Rungwe, Mbeya vijijini, Kiteto, Mufindi, Songea, Iramba, Nyamagana, Ilemela na Ukerewe. Miche 12,000 ya miti malisho ya Leucaena pallida na 12,000 ya Gliricidia sepium imeoteshwa katika vituo vya Kongwa na Mpwapwa kwa lengo la kuisambaza kwa wafugaji wa wilaya za Singida vijijini na Kongwa.

(ii) Uzalishaji, Usambazaji na Tathmini ya Chanjo mbalimbali za Mifugo

Utafiti kuhusu ugonjwa wa kideri (Newcastle disease) katika kuku uliendelea kuhusu uhifadhi na matumizi ya dawa ya chanjo dhidi ya ugonjwa huo. Uzalishaji wa chanjo hiyo umeongezeka kutoka dozi **milioni 6.8** mwaka 2006 na kufikia dozi **milioni 33** mwaka 2009 na kufanya chanjo iliyozalishwa kipindi hicho kufikia dozi milioni **65.7** na kusambazwa kupitia Vituo vya Kanda vya Uchunguzi wa Maradhi ya Mifugo (VIC's). Matumizi ya chanjo hii yamepunguza vifo vya kuku kutoka asilimia **90** hadi **4**.

Utafiti wa tathmini juu ya faida kwa mfugaji wa kuku wa asili zitokanazo na kuchanja dhidi ya ugonjwa wa mdondo kwa kutumia chanjo stahimilifu joto ya I-2 katika mikoa ya Singida, Iringa na Tanga utafiti ulionesha kuwa wafugaji wanafurahia matumizi ya chanjo ya I-2 kwani kuku wa asili wameongezeka kutokana na kupunguwa vifo vinavyosababishwa na ugonjwa wa mdondo. Kuku wameongezeka kutoka idadi ya awali ya kuku **0-5** na kufikia kuku **20** hadi **80** kwa kutumia chanjo ya I-2. Kuongezeka kwa idadi ya kuku kumeongeza kipato kwa mfugaji na pia lishe bora kwa kaya. Hadhi ya akina mama katika kaya nayo imeongezeka hasa wale waliochaguliwa kuwa wachanjaji wa kuku katika jamii zao.

Utafiti wa magonjwa ya Kimeta, Chambavu na Ugonjwa wa Midomo na Miguu unaendelea ambapo dozi **1,765,500** za Kimeta na dozi **336,400** za Chambavu zimezalishwa. Aidha, dozi **8,000** za chanjo ya kuzuia ugonjwa wa kutupa mimba zinafanyiwa majaribio ya ubora na usalama. Maandalizi ya kuanza kutengeneza chanjo dhidi ya Ugonjwa wa RVF yamekamilika. Chanjo kwa ajili ya majaribio tayari imeashaanza kutengenezwa.

(iii) Uchunguzi na Uhakiki Ubora wa Mazao ya Mifugo, Vyakula vya Mifugo pamoja na Mabaki ya Dawa na Sumu.

Maabara Kuu ya Mifugo (CVL) – Temeke ilifanya uchunguzi na kuhakiki ubora wa vyakula vya mifugo ambapo zaidi ya sampuli **4,775** za vyakula vya kuku kutoka kwa wafugaji binafsi, mashamba ya ufugaji na viwanda. Uchunguzi ulionyesha udhafifu tofautitofauti katika ubora wa vyakula hivyo hasa kuhusiana na protini na kabohaidreti. Aidha, wahusika walipewa elimu na ushauri juu ya utengenezaji wa chakula bora.

Aida sampuli zaidi **741** za mazao ya mifugo kama vile nyama na maziwa zilikusanywa kutoka kwa wazalishaji na kuchunguzwa ubora wake. Pia elimu kwa wadau wa uzalishaji wa maziwa,ilitolewa kwa kuwa uchunguzi wa awali ulionyesha kuwa, maziwa katika vibanda vya kuuzia maziwa sio safi kwani yalionekana kuwa na vimelea vya aina ya Staphyloccocus na pia yalikuwa na mabaki ya dawa za tiba(Antibiotics). Asilimia **81** ya Staphyloccocus spp katika maziwa vilikuwa sugu dhidi ya dawa ya penisilini.

3.1.13 Huduma za Ugani wa Mifugo

Utoaji wa huduma za ugani kwa wafugaji ni njia mojawapo ya kuwapatia wafugaji teknolojia sahihi na mbinu za ufugaji bora na huduma hizi hutolewa kwa kiasi kikubwa na Halmashauri za serikali za Mitaa na wadau wengine. Hata hivyo, huduma hizi hazitoshelezi kutokana na upungufu wa wataalam wa mifugo waliopo **13,469** katika ngazi ya vijiji. Ili kupunguza pengo hilo, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa na vyuo iliongezeka kutoka **765** (2006) hadi kufikia **1,222** (2009). Jumla ya wanafunzi **1,580** walihitimu katika kipindi cha kwa miaka minne. Katika mwaka 2009/2010 Wizara inagharamia mafunzo ya stashahada **744** na astashahada **481** kwa wanachuo katika vyuo vya mafunzo ya mifugo vya Tengeru, Mpwapwa, Morogoro, Madaba, Temeke na Buhuri. Katika mwaka 2010/2011 Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa jumla ya wataalam **1,500** katika vyuo hivyo.

Jumla ya wafugaji **71,121** nchini walipatiwa mafunzo kuhusu ufugaji wa kisasa na wa kibiashara katika vyuo vya mifugo na vile vya maendeleo ya wananchi (FDCs) na wakulima (FTCs). Pia, mafunzo kwa wafugaji yametolewa kupitia mashamba darasa **2,164** (Farmer Field Schools - FFS) katika Halmashauri za Serikali za Mitaa **119**. Pia, wakufunzi **118** kutoka Halmashauri **26** walipata mafunzo kuhusu mbinu shirikishi ya shamba darasa la mifugo ili waweze kuanzisha mashamba darasa katika Halmashauri za wilaya za Korogwe, Kilindi, Same, Hai, Arusha, Meru na Karatu Mtwara, Masasi, Tandahimba, Nachingwea, Shinyanga, Ilemela, Bahi, Morogoro, Uyui, Uambo, Nzega, Ngorongoro, Meatu, Mvomero, Misungwi na Manispaa ya Tabora.

Vipeperushi **356,500**, mabango **60,852** na nakala za vijitabu **33,400** kuhusu ufugaji bora vilichapishwa na kusambazwa kwa wadau. Aidha, nakala **2,000** za Kanuni za ufugaji bora zilichapishwa na **1,815** zimesambazwa kwa wadau. Vipindi **210** vya redio na **40** vya Televisheni viliandaliwa na kurushwa hewani na TBC Taifa na TBC 1.

Jumla ya vikundi **1,820** vya wafugaji vimeundwa na vinajihusisha na ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa (Mbeya, Arusha na Tanga), uboreshaji ng'ombe wa asili (Morogoro, Dodoma, Mwanza na Shinyanga), mbuzi wa maziwa (Arusha na Manyara), kuku wa asili (Dodoma na Singida), kuku wa kisasa (Morogoro na Mwanza), kondoo (Arusha na Manyara), udhibiti wa ndorobo (Tanga), nguruwe (Rukwa) na sungura Morogoro na Mtwara.

3.2 Sekta ya Uvuvi

3.2.1 Kuimarisha Udhibiti wa Uvuvi Haramu na Biashara za Magendo ya Mazao ya Uvuvi

(i) Mpango wa Kikanda (Regional Plan of Action) kwa ajili ya udhibiti uvuvi haramu (Illegal, Unreported and Unregulated Fishing -IUU) katika Ziwa Victoria umepitishwa na nchi zote tatu za Kenya, Uganda na Tanzania. Utekelezaji wa Mpango huo utachangia kuwa na rasilimali endelevu katika Ziwa Victoria.

(ii) "Standard Operating Procedures" (SOPs) kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu katika Ziwa Victoria zimekamilika, kukubaliwa na zinatumika katika nchi zote tatu zinazomiliki ziwa hilo.

(iii) Kanuni za Uvuvi wa Mamlaka ya Uvuvi katika Bahari Kuu za 2009 (Deep Sea Fishing Authority Regulations of 2009) zilikamilishwa hivyo kuwezesha utekelezwaji wa Sheria ya Uvuvi ya Mamlaka ya uvuvi katika Bahari Kuu ya mwaka 1998 na marekebisho yake ya 2007. Kukamilika kwa Kanuni hizo kumepelekea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) hivyo kupatiwa ufumbuzi wa suala la uvuvi wa bahari kuu lililokuwa moja ya kero za muungano.

(iv) Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005 zimepitiwa na kutengenezwa kanuni mpya za uvuvi za mwaka 2009. Katika kanuni mpya baadhi ya mambo yaliyoboreshwa ni kuongezwa kwa maduhuli (royalty) na ada za leseni za uvuvi na biashara za mazao ya uvuvi ambazo zitasaidia kuongeza mapato yatokanayo na mazao ya uvuvi.

(v) Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imefanya jumla ya doria 35,069 katika anga (ndege) kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari (Exclusive Economic Zone - EEZ), nchi kavu, mipakani, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa J. K. Nyerere, masoko na mialo ya samaki, Maziwa Makuu, Mabwawa na Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi. Doria hizo zimewezesha kukamatwa zana haramu **461,725**, baruti **196**, samaki wachanga kilo **254,742**, samaki wabichi kilo **26,233**, majongoo bahari kilo **1,441**, dagaa kilo **49,755**, samaki wa baruti kilo **342**, samaki wakavu kilo **50,110**, samaki aina ya sato waliovuliwa kwa sumu kilo **2,037**, mitumbwi **1,451**, injini za boti **158**, baiskeli **48**, na magari **90**. Jumla ya watuhumiwa **8,278** walikamatwa kwa makosa mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuvua bila leseni za uvuvi, kutumia vyombo visivyosajiliwa

katika shughuli za uvuvi, kufanya biashara ya mazao ya uvuvi bila ya leseni, kuvua kwa kutumia baruti na kuvua kwa kutumia zana zisizoruhusiwa ambapo jumla ya kesi **126** zilifunguliwa mahakamani.

(vi) Aidha katika doria ya pamoja iliyofanywa kwa kushirikiana na nchi za SADC kwa meli ya Afrika ya kusini Sarah Baartman; meli moja kubwa ya uvuvi (TAWARIQ 1) ilikamatwa ikivua katika ukanda wa kiuchumi wa bahari ambapo nahodha na mabaharia wa meli hiyo walikamatwa na kufikishwa mahakamani na pia tani 292.7 za samaki aina ya jodari walikamatwa. Samaki hao waligawiwa bure kwa wananchi kupitia taasisi mbalimbali kwa idhini ya mahakama.

(vii) Ili kuongeza ufanisi katika kudhibiti uvuvi haramu Wizara ilianzisha vituo **12** vipya vya doria. Vituo hivyo vimeanzishwa Mtwara, Mafia, Kilwa (Lindi), Horohoro (Tanga), Kipili na Kasanga (Rukwa), Sota na Sirari (Mara), Kasumulo na Tunduma (Mbeya), Kabanga na Kanyigo (Kagera). Aidha maboti **21** na injini zake yalinuliliwa kwa ajili vituo hivyo vipya pamoja na **6** vya zamani kama ifuatavyo.

(viii) Katika kipindi hicho cha miaka minne Wizara ilikusanya maduhuli ambapo makusanyo yalikuwa kama ifuatavyo;

- Mwaka wa 2006 – Jumla ya Tshs 9,671,221,347.00
- Mwaka wa 2007 – Jumla ya Tshs 9,889,421,713.00
- Mwaka wa 2008 – Jumla ya Tshs 8,304,145,544.00
- Mwaka wa 2009 – Jumla ya Tshs 6,584,491,640.90

(ix) Mwongozo wa Kitaifa wa Uboreshaji na Uendeshaji wa Vikundi vya Ulinzi wa Rasilimali ya Uvuvi (Beach Management Units - BMUs) umekamilika na unatumika. Aidha, muundo wa BMUs katika Ziwa Victoria umeboreshwa kwa kushirikisha wadau wote. ambapo jumla ya vikundi **433** vimeimarishwa. Jumla ya vikundi **170** vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi vimeanzishwa ambapo vikundi **29** Bwawa la Mtera, **19** Bwawa la Nyumba ya Mungu, **11** Mto Ruhuhu. Vilevile jumla ya vikundi vya usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi **111** vimeanzishwa katika Ukanda wa Pwani. Mkutano wa wadau wa sekta ya Uvuvi ulifanyika na wadau walitoa mapendekezo mbali mbali juu ya sekta ya uvuvi.

(x) Rasimu ya kuanzisha maeneo ya usimamizi wa pamoja (Guidelines for Establishment Collaborative Fisheries Management Areas) imeandaliwa kwa kushirikiana na "World Willdlife Fund - WWF" ambapo maeneo **3**

yameanzishwa ambayo ni Wilaya ya Mafia, Wilaya ya Rufiji na Wilaya ya Kilwa.

(xi) Sensa ya uvuvi pia imefanyika katika Maziwa ya Kitangiri, Manyara na jipe. Aidha, Ziwa Kitangiri lina jumla ya wavuvi **457** na vyombo vya uvuvi **224.** Ziwa manyara lina jumla ya wavuvi **202** wanaotumia vyombo **91** ambapo Ziwa jipe lina jumla ya wavuvi **78** na vyombo **50**.

3.2.2 Kuimarisha Ubora na Usalama wa Samaki na Mazao ya Uvuvi

(i) Ujenzi wa Maabara ya Taifa ya Nyegezi ya Udhibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi umekamilika. Maabara hiyo ilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, mwezi Januari, 2007. Vifaa vya kisasa vya maabara vyenye thamani ya takriban shilingi **bilioni 1.33** vilinunuliwa. Maabara hiyo imepata ithibati **Na. T 0327** iliyotolewa na South African National Accreditation Services (SANAS) na hivyo kutambulika Kimataifa.

(ii) "Standard Operating Procedures, "Code of Practices" na "Fish Inspectors' Guide" kwa ajili ya kuthibiti usalama na ubora wa mazao ya uvuvi zimekamilika na zinatumika katika nchi za Kenya, Uganda na Tanzania.

(iii) Kutokana na kukidhi viwango vya ubora vya kimataifa, samaki aina ya kamba wanaofugwa katika Wilaya ya Mafia wamepata soko la nje katika nchi za Jumuiya ya Ulaya.

(iv) Mialo **19** imekarabatiwa na **6** mipya imejengwa katika ukanda wa Ziwa Victoria.

(v) Jumla ya sampuli **5,413** kutoka Ziwa Victoria na viwanda **18** vya kuchakata samaki vya ukanda wa Ziwa Victoria na ukanda wa Pwani vilifanyiwa uchunguzi katika maabara za ndani na nje ya nchi ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao hayo na mazingira yake. Matokeo yalionyesha kuwa sampuli zote zilikuwa nzuri. Pia, meli **15** za uvuvi zilikaguliwa na maeneo **15** ya kutunzia samaki hai na maghala **11** ya kuhifadhia mazao makavu ya uvuvi yalikaguliwa.

(vi) Wataalam **73** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na wavuvi **1,586** walipata mafunzo kuhusu njia endelevu za uchakataji na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi.

3.2.3 Kuendeleza Ukuzaji wa Viumbe Kwenye Maji

Wizara imeendelea kuhimiza ukuzaji wa viumbe hai kwenye maji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa samaki na mazao mengine ya majini. Hadi sasa yafuatayo yamefanyika:

- Kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Uendelezaji wa Ukuzaji wa Viumbe Kwenye Maji (National Aquaculture Development Strategy).

- Kuboresha vituo **8** vya kuendeleza ukuzaji wa viumbe kwenye maji ambavyo ni Ruhira (Songea), Kilimanjaro, Sikonge (Tabora), Mtama (Lindi), Kagera, Musoma, Mwanza na Kingolwira (Morogoro).

- Kituo cha Kingolwira (Morogoro) kimeboresha teknolojia ya ufugaji wa samaki aina ya kambale kwa kuongeza muda wa kuishi (survival rate) wa vifaranga wa kambale kutoka asilimia **5** hadi kufikia **40**.

- Vituo vya Kingolwira na Mbarali vimezalisha na kusambaza vifaranga **1,799,380** aina ya perege na **9,832** aina ya kambale kwenye mabwawa ya kuchimba katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Tabora, Iringa, Manyara, Kilimanjaro, Mbeya na kupandikiza vifaranga **624,571** kwenye malambo ya asili katika mikoa ya Dodoma, Tanga Pwani, Rukwa, Iringa, Tabora. Shinyanga, Mara, Pwani, Kilimanjaro na Morogoro.

- Vituo vya ukuzaji wa viumbe kwenye maji vya Mikoa ya Kagera, Mwanza, na Mtama (Lindi) vimechimba mabwawa ya mfano yanayotumika kama mashamba darasa kwa ajili ya wafugaji wa samaki katika maeneo hayo

- Kuboresha Ufugaji wa Kambamiti kibashara unaofanywa na Kampuni ya Alphakrust Wilayani Mafia. Mradi huo una mabwawa **30** yenye ukubwa wa wastani wa hekta moja na nusu kila bwawa na uwezo wa kuzalisha kambamiti ni wastani wa **tani 912** kwa mwaka zenye thamani ya Dola za Kimarekani **milioni 8.5** kama mabwawa yote **76** yanayotegemewa kuchimbwa yatatumika. Hadi sasa mradi umezalisha **tani 374.5** zenye thamani ya takribani Dola za Kimarekani **2,351,880**.

- Kampuni ya PRAWNTO kwa kushirikiana na Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani imefanya majaribio ya kuzalisha mbegu za kambamiti. Majaribio

haya yameonyesha mafanikio na jumla ya vifaranga **75,000** vya kambamiti (post – larvae) vimesambazwa mwezi Agosti, 2009 kutoka katika kituo hicho kwenda Mkoa wa Tanga kwenye vijiji vinne vya Kibindani (**10,000**), Kigombeni (**40,000**), Ndaoya (**5,000**) na Chongoleani (**20,000**). Kati ya vifaranga vilivyopandikizwa, kilo **101.5** zenye thamani ya **shilingi 507,500** zimevunwa. Jumla ya vijiji **21** vimeainishwa kuwa vinafaa kwa ajili ya ufugaji wa kambamti katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani. Mafunzo ya kuboresha ufugaji wa kambamti yametolewa kwa wanakijiji **783** katika Mikoa ya Lindi, Pwani na Tanga.

- Kilimo cha Mwani katika maeneo ya ukanda wa pwani kinahusisha wakulima takribani **3,000**. Katika kipindi hicho, **tani 1172.9** zimezalishwa, bei ya mwani mkavu ni kati ya **shilingi 220/=** hadi **400/=** kwa kilo. Mwani unaozalishwa unauzwa nchi za nje kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwenye viwanda. Vijiji **14** katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani vimeainishwa kwa ajili ya kilimo hicho. Vikundi **8** vinavyojishughulisha na ukulima wa mwani katika Wilaya za Pangani, Mkuranga, Kilwa, Mkinga na Tanga vimefadhiliwa kwa kupewa fedha na Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (MACEMP) kupitia mfuko wa jamii wa vijiji vya pwani. Pia mafunzo ya kuboresha kilimo cha mwani yametolewa kwa wanavijiji **864** katika Mikoa ya Lindi, Pwani na Tanga.

- Vilevile Mradi wa Usimamizi wa Mazingira kupitia shughuli za ukuzaji viumbe kwenye maji bahari (SEMMA) umeingia mkataba na "MACEMP" Kuendeleza kilimo cha mwani katika Mkoa wa Tanga Wilaya ya Mkinga, kijiji cha Kijiru na kupewa **shilingi 62,537,930** za uendeshaji. Hadi sasa, fedha hizo zimetumika kujengea ghala la kuhifadhia mwani, madau yote kumi yametengenezwa, kamba **2,250** zenye urefu wa mita **20** zimegawiwa kwa wakulima **45** na mafunzo ya usimamizi wa kikundi yametolewa na "Rural Resource Center" (RRC) kutoka Wilayani Lushoto.

- Mkataba wa aina hiyo pia umefanywa na kampuni ya Nyamwese, Mkoa wa Pwani Wilaya ya Mafia kijiji cha Jibondo na kupewa **shilingi 64,464,661** za uendeshaji. Kutoka kwenye fedha hizo, ujenzi wa jengo la kuhifadhia zao la mwani bado haujaanza bali eneo na ramani ya jengo vipo tayari, kikundi tayari kimepata elimu juu ya uongozi (leadership skills) na elimu juu ya mbinu za kilimo cha mwani kwenye kina kifupi na kirefu bado haijatolewa kama mkataba wa makubaliano unavyosema.

- Ufugaji wa Samaki aina ya Mwatiko unahusisha zaidi ya mabwawa **70** yenye wastani wa ukubwa wa mita mraba 20x30 (600m2). Kilo **370** zenye thamani ya **shilingi 1,295,000** zimezalishwa. Hadi sasa, jumla ya vijiji **21** vimeainishwa kuwa vinafaa kwa ajili ya ufugaji wa mwatiko katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani. Mafunzo ya kuboresha ufugaji wa mwatiko yametolewa kwa wanakijiji **783** katika Mikoa ya Lindi, Pwani na Tanga.

- Unenepeshaji wa Kaa unafanyika katika Wilaya za Rufiji (Pwani) na Pangani (Tanga) ambapo kuna vizimba **204**. Kwa kipindi hicho tani **5,000** za kaa wenye thamani ya **shilingi 25,000,000** zimevunwa katika Wilaya ya Pangani. Pia jumla ya vijiji **21** vimeainishwa kuwa vinafaa kwa ajili ya unenepeshaji kaa katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani. Mafunzo ya kuboresha unenepeshaji wa kaa yametolewa kwa wanavijiji **783** katika Mikoa ya Lindi, Pwani na Tanga.

- Majaribio ya ukuzaji wa lulu yanafanywa na baadhi ya wanavijiji kwa kufadhiliwa na Shirika la "World Wide Fund" (WWF) katika Wilaya ya Mafia na lulu **400** kutoka kwenye chaza zenye thamani ya **shilingi 13,000,000** zilivunwa. Majaribio haya pia yanafanyika katika Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani ambapo jumla ya "nuclei" **200** zimepandikizwa kwenye kaka la chaza kwa ajili ya kukuza lulu.

3.2.4 Kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania - TAFIRI

- TAFIRI kupitia vituo vyake vya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Kyela na kituo kidogo cha Sota mkoani Mara iliendelea kufanya utafiti wa kubaini uwingi wa samaki kwenye maji ya kina kifupi katika Bahari ya Hindi na ufugaji wa samaki aina ya mwatiko (*milk fish*) katika wilaya za Kilwa, Rufiji na Mafia. Aidha, mabwawa ya mfano ya kufuga samaki aina ya mwatiko yamejengwa kwenye Chuo cha Mbegani (Bagamoyo) na Kilongawima (Kinondoni) kwa ajili ya mafunzo kwa wafugaji wa samaki.

- Taasisi imeendelea kushirikiana na idara ya Uvuvi na Taasisi nyingine za Kenya na Uganda katika utekekelezaji mradi wa usimamizi menejimenti ya Ziwa Victoria. Lengo kuu la mradi wa IFMP ni kuinua uhifadhi, uendelezaji na Uvunaji endelevu wa rasilimali ya uvuvi katika Ziwa Victoria kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo. Mradi unatekelezwa na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda ambazo humiliki Ziwa Victoria. Mradi ulianza mwaka 2003 chini ya ufadhili wa Umoja wa nchi za Ulaya (EU) kwa gharama ya Euro **milioni 29.9** na kukamilika mwaka 2008. Utafiti umebaini kuwa uwingi wa samaki aina ya sangara umepungua kutoka **tani 700,690**

mwezi Februari 2005 na kufikia **tani 227,365** mwezi Agosti 2008. hata hivyo mwezi Agosti 2009, sangara wameongezeka kidogo na kufikia **tani 307,539**. Aidha, TAFIRI ilifanya sensa ya uvuvi katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Bahari ya Hindi na Bwawa la Mtera na kubaini yafuatayo:

- Katika Ziwa Victoria idadi ya wavuvi imeongezeka kutoka **98,015**, mwaka 2005 hadi **105,019** mwaka 2008. Vyombo vya uvuvi (mitumbwi) kutoka **29,732** hadi **30,206** na kuwepo kwa nyavu aina mbalimbali **931,889** na mialo **634.**

- Taasisi vilevile imeanza kutathmini uwingi, mtawanyiko na aina za samaki waliopo kwenye bahari ya hindi. Baada ya kuangalia takwimu za mwelekeo wa uvuvi wa kambamiti, uwingi wa kambamiti ulipungua kutoka **tani 1,320.1** mwaka 2003 hadi **tani 202.5** mwaka 2007. Taasisi iliishauri serikali kupunguza idadi ya meli zitakazopewa liseni kutoka **22** na kufikia **17** musimu wa mwaka 2007 na kuzuia uvuvi wa kambamiti kwa meli kubwa za kibiashara katika ukanda wa pwani ili wazalianena kufanya mazingira na mazalio yao na ya samaki kuboreka zaidi nakuelekeza uvuvi sehemu nyingine ambayo rasilimali yake bado haijavunwa kikamilifu. Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) imeendelea kufanya utafiti wa ufuatiliaji wa mwenendo wa rasilimali ya kambamiti ili kutathmini uwingi baada ya kufunga uvuvi huo kwa wavuvi wa meli kubwa na za kati mwaka 2008. Matokeo ya ufuatiliaji huo yameonyesha kwamba Kambamiti wameanza kuongezeka kutoka **tani 19.1** mwaka 2004 na kufikia **tani 920** mwaka 2009 kwa zoni 1; na kutoka **tani 95.5** mwaka 2004 na kufikia **tani 920.2** mwaka 2009 kwa zoni 2.

- Utafiti wa rasilimali ya uvuvi katika ziwa Kitangiri na Bwawa la Nyumba ya Mungu umeonesha kuwa kuna jumla ya wavuvi **358** wenye mitumbwi **179** katika Ziwa Kitangiri. Jumla ya **tani 844.4** za samaki zenye thamani ya **shilingi 463,164,853** zilivuliwa mwaka 2009. Vile vile, Katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, TAFIRI inafanya utafiti wa kubaini maeneo ya mazalio ya samaki. Sababu za kuvia na kuzaa katika umri mdogo kwa samaki aina ya Oreochromis esculenta waliopandikizwa toka Ziwa Victoria zimejulikana kuwa ni kukosekana kwa chakula cha samaki huyo. Aidha, suala la kupungua kwa maji katika bwawa hilo ni suala mtambuka.

3.2.5 Kuimarisha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu

Taasisi ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu iliendelea na kazi ya kusimamia rasilimali za bahari na pwani ili kuhakikisha kuwa matumizi endelevu ya rasilimali

za bahari na mwambao yanafanyika. Katika kipindi hicho yafuatayo yametekelezwa:-

(i) Kukuza uelewa na utalii wa kimazingira (utalii ikolojia – eco-tourism) kwa wananchi kuhusu dhana ya uhifadhi wa bahari na maeneo ya fukwe.

Mafunzo ya uhifadhi bora wa bahari na maeneo ya pwani yalitolewa kwa wananchi waishio ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Takriban jumla ya wananchi wapato **12,000** walipata mafunzo. Aidha, nyenzo mbalimbali za kujenga ufahamu juu ya uhifadhi yakiwepo majarida na vipeperushi, viliandaliwa na kusambazwa kwa wananchi. Jumla ya vipeperushi **35,500** vilitengenezwa. Vipindi **25** vya redio na runinga viliandaliwa na kurushwa hewani. Pia, Taasisi imeshiriki maonyesho **matano** ya ndani na onyesho moja la utalii la kimataifa la Indaba huko Afrika ya kusini.

(ii) Kuwezesha shughuli mbadala ili kupunguza utegemezi kwenye shughuli za uvuvi.

Juhudi za kupunguza kasi ya uharibifu wa rasilimali za bahari ziliendelea kuimarishwa kupitia mpango wa ubadilishanaji wa zana haribifu kwa zana bora na pia kwa kuwezesha shughuli mbadala. Jumla ya wananchi 850 waliwezeshwa kufanya shughuli mbadala na pia kupewa zana bora za uvuvi. Shughuli mbadala zilizofanyika ni pamoja na ufugaji nyuki, ufugaji samaki na kaa, ukulima wa mwani, ukulima wa mboga mboga, utalii ulio rafiki na mazingira, utengenezaji wa batiki na ususi.

(iii) Kuendelea kutenga maeneo ya uhifadhi.

Eneo moja la mwambao wa Tanga limetangazwa kuwa Hifadhi mpya ya Silikanti tangu Agosti 2009. Jumla ya visiwa sita **(6)** vilitengwa na kutangazwa kuwa Maeneo Tengefu. Visiwa hivyo ni pamoja na Sinda, Kendwa na Makatube vilivyoko Dar es Salaam na Nyororo, Mbarakuni na Shungimbili vilivyoko kwenye ukanda wa bahari Mafia na kuyafanya maeneo ya aina hiyo kuwa kumi na moja. Taarifa muhimu (biophysical and social economics surveys) zimekusanywa ili kutumika katika uandaaji wa mipango ya jumla ya usimamizi wa maeneo hayo.

Juhudi zinafanyika za kuanzisha Hifadhi ya Bahari ya tatu kwenye Mwambao wa Tanga itakayohifadhi samaki aina ya Silikanti na viumbe wengine wa baharini. Majadiliano na wadau wa maeneo hayo kwa kupitia mikutano ya hadhara yamefanyika na wadau wa eneo hilo wameridhia ili eneo hilo kuwa Tengefu.

Taarifa za kisayansi zimepatikana zitakazowezesha mchakato wa kulitangaza eneo hilo kuwa hifadhi. Pia tumeainisha visiwa vingine **4** vya Ulenge, Kwale, Mwewe na Kirui vilivyoko Kaskazini ya mji wa Tanga kuwa Maeneo Tengefu. Tayari tumechukua alama za mipaka ya visiwa hivyo zitakazowezesha maandalizi ya andiko litakalovitenga kisheria kuwa maeneo yaliyohifadhi (gazzettment notice).

(iv) Kufanya mapitio ya Sheria iliyoanzisha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu

Mchakato wa kuimarisha Taasisi kutoka kwenye muundo wa sasa ambao unakanganya na kuweka muundo unaoeleweka wa kuwa Taasisi inayojitegemea moja kwa moja kimadaraka unafanyika. Hii inahusisha kufanya marejeo ya Sheria Na. 29 ya mwaka 1994 iliyoanzisha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Kazi ya kufanya marejeo ya Sheria imeanza na inatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwaka huu.

Taasisi pia imeweza kuandaa machapisho ya Kanuni mbali mbali za Hifadhi za Bahari na maeneo Tengefu kwa ajili ya kuwezesha Mipango ya Ujumla ya usimamzi wa Hifadhi za Bahari na maeneo tengefu ili uweze kufanya kazi kisheria.

(iv) Kuendeleza mpango wa kubadilishana zana haribifu kwa zana bora za uvuvi endelevu ili kupunguza kasi ya uharibifu wa rasilimali za bahari.

Wananchi **654** wanaoishi ndani ya maeneo ya hifadhi wamefaidika na mpango huo ambapo wamepatiwa mashine za kupachika **12**, masanduku **4** ya barafu (ice boxes) kwa ajili ya kuhifadhia samaki, nyavu za jarife vipande **1,214** pamoja na maboti **10**. Boti na mashine zilizotolewa zinawawezesha wavuvi kuvua kwenye maji ya kina kirefu na hivyo kupunguza nguvu ya uvuvi kwenye Bahari ya Ndani (Territorial waters).

Kuendeleza uhifadhi shirikishi kwenye maeneo tengefu ya Bongoyo, Mbudya na Sinda ambapo jumla ya vikundi vitatu vya wanajamii vyenye walinzi **40** wa rasilimali za bahari na mwambao vimeanzishwa. Vikundi hivi vimepatiwa boti na injini kufanya doria kudhibiti uvuvi haribifu.

3.2.6 Mafunzo ya Wataalam na Wavuvi

Mafunzo ya wataalam wa uvuvi yameendelea kutolewa katika Vyuo vya Uvuvi vya Mbegani na Nyegezi. Katika kipindi cha miaka minne wanafunzi waliodahiliwa ni **780** na waliohitimu ni **432**. Katika kipindi hicho, wanafunzi waliodahiliwa na vyuo iliongezeka kutoka **110** hadi kufikia **293**.

Wataalam wa ugani waliopo ni **540**, ikilinganishwa na mahitaji ya wagani **16,000**. Aidha, mafuzo yameendelea kutolewa kwa wamiliki wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi **124** katika ukanda wa Ziwa Victoriana wafanya biashara **430** katika wilaya za Rufiji, Kilwa na Mafia juu ya usafirishaji, uchakataji na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi.

Elimu ya kazi mbadala ili kupunguza utegemezi kwenye uvuvi ilitolewa kuhusu ufugaji nyuki kwa wanajamii **160**, ufugaji wa samaki wanavijiji **156**, ufugaji wa kuku kwa wanajamii **70** na ukulima wa mwani kwa wanjamii **80**. Wanajamii waliwezeshwa kufanya shughuli hizo. Pia, mafunzo ya utalii rafiki wa mazingira yalitolewa kwa wanavijiji **55** wanajighulisha na shughuli za utalii.

Nyenzo za kuwezesha elimu ya mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari ziliandaliwa. Jumla ya vipeperushi **40,300** na vipindi **50** vya redio na **20** vya luninga vilitengenezwa na kurushwa hewani. Pia, elimu dhidi ya uvuvi haramu na athari zake ilitolewa kwa wavuvi mkoani Tanga na viongozi wapatao **2,655** nao walihamasishwa kusimamia uanzishwaji wa BMUs kwenye maeneo yao.

3.2.7 Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (Marine and Coastal Environment Management Project - MACEMP)

Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani unaofadhiliwa na Benki ya Dunia unatekelezwa katika visiwa vya Unguja na Pemba kwa upande wa Zanzibar na kwa upande wa Tanzania Bara unatekelezwa katika Halmashauri **16** katika Wilaya zote **14** za ukanda wa Pwani kwa kipindi cha miaka **6** kuanzia Desemba 2005 hadi Desemba 2011. Kwa upande wa Tanzania Bara, Mradi ulitengewa kiasi cha Dola za Kimarekani **millioni 35** kwa kipindi cha miaka **6**. Tangu utekelezaji wa Mradi uanze hadi kufikia December, 2009 jumla ya Dola za Kimarekani **milioni 18.96**, sawa na asilimia **54** ya fedha zote zimekwishatumika. Hadi sasa, Mradi wa MACEMP umetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

(i) Kuwezesha kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Shughuli za Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

- Sheria Na. 6 ya mwaka 2007 ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu (Deep Sea Fishing Authority) imetungwa na Kanuni zake za mwaka 2009;
- Kuteuliwa kwa Timu ya mpito ya watekelezaji wa Mamlaka;
- Kuteuliwa kwa Mtendaji Mkuu (Mkurugenzi Mkuu) wa mamlaka,
- Kuwezesha uendeshaji wa doria za anga na baharini katika eneo la Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola (Jeshi la Majini na Askari Polisi wanamaji). Kukamatwa kwa chombo cha uvuvi haramu MV. TAWARIQ 1 (Bou Young) ni mojawapo ya matokeo ya doria za Mamlaka kwa kutumia Meli ya SARABATMAN inayomilikiwa na Serikali ya Africa Kusini. Kesi bado ipo Mahakamani;
- Kuwezesha kuwekwa kwa Mfumo wa kudhibiti meli za kigeni (the Vessel Monitoring System) zinazovua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu. Mtambo wa Mfumo huu sasa umehamishiwa Zanzibar yalipo Makao Makuu ya Mamlaka; na
- Kuwezesha viongozi na watalaam wa Wizara kushiriki katika mazungumzo na taasisi mbalimbali kikanda na kimataifa ili kujadili mikakati ya uvuvi endelevu.

(ii) Kuwezesha uendeshaji wa doria za nchi kavu na baharini, kwa lengo la kudhibiti uvuvi na shughuli haramu zinazoathiri rasilimali ya uvuvi, pamoja na mazingira yake

- Jumla ya watumishi **107** walipatiwa mafunzo ya udhibiti na doria chini ya ufadhili wa Mradi wa MACEMP, na
- Kuwezesha kufanyika kwa mikutano mbalimbali ya kufahamisha wadau juu matakwa ya Sheria ya Uvuvi na Kanuni zake, pamoja na athari za uvuvi haramu.

(iii) Kuimarisha usimamizi wa eneo la bahari ya ndani na ya kitaifa kwa kuwezesha ushiriki wa jamii zinazoishi katika maeneo hayo

- Kuwezesha Halmashauri lengwa kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Mradi katika ngazi ya Halmashauri;
- Kusaidia Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi (TAFIRI) kufanya tathmini ya wingi na aina ya samaki katika maji ya kitaifa na ndani. Taarifa za kitafiti

zinaonyesha kuwa nguvu ya uvuvi inaongezeka kwa kasi mwaka hadi mwaka na kwamba rasilimali ya uvuvi inaendelea kupungua; na

- Mradi umesaidia kuhamasishwa kwa jamii za wavuvi kuunda vikundi vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi ("Beach Management Unit" - BMUs) katika Halmashauri za mwambao wa Pwani. Jumla ya vijiji **177** vilihamasishwa kuanzisha vikundi hivyo. Mchakato wa kuunda vikundi katika Halmashauri hizi upo katika hatua mbalimbali.

(iv) Kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi timilifu wa Mazingira ya Pwani (Integrated Coastal Management Strategy - ICM)

- Kupitia Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Mradi umejenga uwezo wa jamii katika suala la usimamizi timilifu wa mazingira ya pwani na bahari kwa kutoa mafunzo, ambapo jumla ya viongozi **1,359** wakiwemo madiwani, watendaji wa kata na vijiji walishiriki,
- Kutokana na mafunzo haya halmshauri zote **16** za mwambao wa pwani zipo katika hatua tofauti tofauti za mchakato wa kuandaa Mipango ya Usimamizi Timilifu wa Mazingira ya Pwani (ICM Plans). Mipango hii itawezesha halmashauri kuweka mipango ya uwiano wa matumizi ya rasilimali za pwani.
- Watumishi **72** wakiwemo madiwani na watumishi wa halmashauri kutoka Halmashauri za mwambao wa Bahari walipewa mafunzo ya Tathmini ya Athari za Mazingira (Enviromental Impact Assessment - EIA) zinazoweza kujitokeza kutokana na shughuli za uchumi na kijamii zinazoendeshwa katika maeneo haya. Mafunzo haya yamewajengea uwezo wa kufanya tathmini za mazingira kwenye miradi midogo midogo ya kiuchumi na kijamii zinazofanyika katika maeneo yao.

(v) Usimamizi wa Malikale na ukarabati wa magofu

- Mradi umewezesha wananchi wa mwambao wa pwani kushiriki kikamilifu kwenye ulinzi na usimamizi wa malikale, yakiwemo maeneo ya kihistoria kama vile magofu, ili yatumike kuinua kipato cha wananchi kupitia kuvutia watalii. Maeneo yote yenye utajiri wa malikale yametambuliwa, na baadhi ya magofu muhimu yanayoweza kuwaletea wananchi kipato, yanafanyiwa ukarabati kwa kuzingatia sheria. Baadhi ya magofu yapo katika maeneo ya Kilwa (Kilwa kisiwani), Mafia Archipelago na Rufiji.
- Katika maeno hayo, Mradi umewezesha kufanyika kwa utafiti wa maarifa asilia (indigeneous knowledge), ambayo ni muhimu katika kuweka mipango ya usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za baharini na pwani, zikiwemo mali kale, mikoko, matumbawe na rasilimali za uvuvi.

(vi) Kuanzisha, kuimarisha na kuendeleza Maeneo Tengefu

- Kuwezesha uanzishaji wa maeneo mengi zaidi ya hifadhi za bahari kwa lengo la kuimarisha uhifadhi wa rasilimali katika maeneo muhimu. Mradi umewezesha kuendelezwa kwa hifadhi mbili za bahari, ambazo ni Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia (the Mafia Island Marine Park (MIMP), na Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi Bay katika Maingilio ya Mto Ruvuma inayojulikana kama "the Mnazi Bay Ruvuma Estuary Marine Park (MBREMP)".

- Maeneo mengine tengefu ambayo yanasimamiawa na Taasisi ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (Marine Parks and Reserve Unit - MPRU) ni visiwa vodogovidogo vilivyoko maeneo ya Dar es salam, ambavyo ni Mbudya, Bongoyo, Sinda, Makatube (inner and outer), Pangavini na Kendwa. Maeneo mengine tengefu ni Maziwe (Pangani), Visiwa vya Nyororo, Shungimbili na Mbarakuni vilivyopo katika kisiwa cha Mafia. Kupitia MPRU, Mradi wa MACEMP umewezesha kufanyika kwa shughuli mbalimbali katika hifadhi za Bahari na maeneo tengefu kama ifuatavyo:

  - Kuanzishwa kwa Hifadhi mpya ya Bahari inayojulikana kama "the Coelacanth Marine Protected Area" iliyopo Mkoa wa Tanga. Hifadhi hii ni maalum kwa kuonekana kwa wingi kwa "Coelacanth" au kwa Kiswahili 'Silikanti'. Eneo hili, ni kivutio kikubwa kwa watalii, wanasayansi na wana harakati wa hifadhi duniani kote;

  - Kufanya doria mbalimbali katika maeneo ya hifadhi;

  - Mpango wa kubadilisha zana za uvuvi rafiki wa mazingira na zana haribifu (the Gear exchange Programme), ili kuwahamasisha wavuvi kuachana na uvuvi haramu na kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za usimamizi wa rasilimali na mazingira yake ulitumia jumla ya shilingi **64,500,000** na jumla ya wananchi **217** walifaidika;

  - Mradi wa MACEMP umewezesha ujenzi wa ofisi ya Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi bay na Maingilio ya Mto Ruvuma Mkoani Mtwara katika eneo la Ruvula Peninsula. Jengo hilo limekamilika mwezi Oktoba 2009;

  - Mradi unawezesha ujenzi wa ofisi ndogo ya utafiti wa viumbe baharini katika Wilaya ya Mafia.

(vii) Kuwezesha jamii za Pwani kuibua na kusimamia miradi midogo

Mradi unatoa fursa kwa jamii za pwani kuibua, kutekeleza na kusimamia miradi midogo midogo inayolenga kuboresha maisha yao na kuweka mfumo-ikolojia ambao ni endelevu. Jumla ya miradi midogo midogo **403** ya wananchi imekwishapatiwa jumla ya **shilingi 5,694,086,419** kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wake. Mchanganuo wa miradi hiyo kwa kila Halmashauri ni kama ifuatavyo:

Na.	Wilaya	Idadi ya miradi	Thamani Tsh	Idadi ya watu		Jumla ya watu
				Me	Ke	
1.	Halmashauri ya Jiji la Tanga	30	463,474,275	280	244	524
2.	Muheza	10	123,828,100	112	56	168
3.	Mkinga	28	427,073,960	251	257	508
4.	Pangani	24	343,098,751	256	143	399
5.	Mkuranga	16	258,101,580	131	106	237
6.	Mafia	56	567,300,560	439	218	657
7.	Kilwa	63	858,961,510	581	389	970
8.	Rufiji	62	757,932,395	759	412	1171
9.	Lindi mjini	9	143,265,528	176	66	242
10.	Lindi vijijini	19	319,070,125	286	139	425
11.	Mtwara Mikindani	16	230,492,400	169	162	331
12.	Mtwara vijijini	15	201,386,375	217	145	362
13.	Bagamoyo	39	758,597,620	446	202	648
14.	Manispaa ya Kinondoni	9	117,102,920	64	66	130
15.	Manispaa ya Ilala	7	124,400,320	112	3	115
	Jumla	**403**	**5,694,086,419**	**4,279**	**2,608**	**6,887**

(viii) Kuwezesha vikundi vya kijamii vya kusimamia mazingira na baioanuwai, kupitia fedha za msaada wa Shirika la Mazingira Duniani (GEF)

Katika msukumo wa kuongeza ari ya wananchi wanaojihusisha na miradi ya kuhifadhi mazingira, Mradi unatoa fedha za kuwezesha vikundi vya kijamii kusimamia kwa nguvu zaidi uendelevu wa baioanuwai, pamoja na mazingira yake. Walengwa wakuu wa eneo hili ni vikundi mbalimbali vyenye kujishughulisha na utunzaji na uhifadhi wa mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani. Jumla ya miradi **33** yenye thamani ya **shilingi 158,609,000** imekwisha idhinishwa kupatiwa fedha kutoka katika Halmashauri za Temeke (**6**), Pangani (**10**), Muheza (**3**), Kinondoni (**6**), Ilala (**1**), na Jiji la Tanga (**7**).

(ix) Kuwezesha mashirikiano ya kibiashara kati ya vikundi vya kijamii na Sekta binafsi

Lengo la kuunganisha makundi haya mawili ni kuwezesha uzoefu wa sekta binafsi kutumika katika kuinua ufanisi wa shughuli za vikundi vya kijamii, ili mwananchi aweze kuboresha kipato chake kutokana na kuuza mazao bora zaidi, kwa wingi zaidi na kwa bei yenye tija. Katika kutekeleza hili, Mradi wa MACEMP uliingia makubaliano na kampuni mbili (SEMMA na Nyamwese Ltd.), kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa mwani katika kijiji cha Kijiru – Wilayani Mkinga, Tanga (SEMMA) na kijiji cha Jibondo Mafia (Nyamwese Ltd).

(x) Kuwezesha upashanaji habari za utekelezaji wa Mradi kwa wadau, kwa kuandaa na kusambaza makala mbalimbali

- Mradi uliendesha semina za viongozi katika ngazi ya wilaya kwa kuwahusisha viongozi wa wilaya, madiwani, wakuu wa Idara kabla ya shughuli za mradi kuanza kutekelezwa. Aidha, kila wilaya iliendesha semina za utambulisho wa Mradi katika ngazi ya Kata na vijiji.
- Mradi unawezesha maandalizi na usambazaji wa vipeperushi mbalimbali vya maelezo ya Mradi kwa wadau wa ngazi zote. Aidha, njia ya redio na televisheni pia hutumika kutangaza habari za meaendeleo ya utekelezaji wa shughuli za Mradi. Aidha, Mradi hufadhili utengenezaji na usambazaji wa fulana na kofia zenye kubeba ujumbe wa MACEMP kwa ajili ya kufahamisha maendeleo ya utekelezaji wa kazi za Mradi kwa wadau,
- Mradi unafadhili ushiriki wa wadau na watekelezaji wake katika sherehe mbalimbali za kitaifa kwa mfano: Siku ya utumishi wa Umma zilizofanyika, sikukuu za nane nane, Siku ya Mazingira na nyingine nyingi.

(xi) Kuwezesha utoaji wa huduma mbambali za kitaalam/ushauri, ununuzi wa vifaa vya mradi, pamoja na ujenzi wa miundombinu

Huduma hizo ni pamoja na ununuzi wa vifaa, zikiwemo samani za ofisi, kompyuta, printa, scanner, vyombo vya usafiri (magari, pikipiki, baiskeli, boti) na vifaa vya ofisi. Aidha, Mradi unawezesha pia kazi za ujenzi zifuatazo: jengo la Idara ya Uvuvi (''Mvuvi House''), ujenzi wa vituo vya biashara vya jamii (Community Business Centres) katika wilaya tatu za Kilwa, Mafia na Rufiji, kuwezesha uboreshaji wa mialo "fish landing sites" katika wilaya tatu za mfano, pamoja na kuwezesha ukarabati na uhifadhi wa malikale chini ya Idara ya Malikale (Antiquities Division).

3.3 Maeneo ya Mtambuka

3.3.1 Sera na Sheria mbalimbali

(i) Sera ya Taifa ya Mifugo

Sera ya Taifa ya Mifugo imeandaliwa na imepitishwa na Serikali tarehe 12 Desemba, 2006. Hadi sasa, jumla ya nakala **5,000** ya sera hiyo katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili zimesambazwa kwa wadau, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu. Waraka wa kuwasilisha rasimu ya mwisho ya Mkakati wa Kutekeleza Sera ya Taifa ya Mifugo (Livestock Sector Development Strategy) umeandaliwa na kuwasilishwa Baraza la Mawaziri kwa hatua zaidi.

(ii) Mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 1997

Rasimu ya mwisho ya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 1997 imekamilika na Waraka wa Baraza la Mawaziri wa kuiwasilisha Serikalini umeandaliwa. Aidha, Hadidu za Rejea za kuandaa Mkakati wa kutekeleza Sera ya Taifa ya Uvuvi zimeandaliwa na kazi ya kuandaa mkakati huo inaendelea.

(iii) Sheria mbalimbali za Sekta za Mifugo na Uvuvi

(a) Sheria zilizokamilika na kutumika ni:

- Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006;
- Sheria ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority Act)* Na. 6 ya mwaka 2007;
- Sheria ya Biashara ya Ngozi (*Hides, Skins na Leather Trade Act*) Na. 18 ya mwaka 2008; na
- Sheria ya Ustawi wa Wanyama (*Animal Welfare Act*) Na. 19 ya 2008.

(b) Mapendekezo ya kutungwa Sheria za Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo (The *Grazing Land and Animal Feed Resources Act*) na Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo (T*he Livestock Identification, Registration and Traceability Act*) yamepitishwa na Baraza la Mawaziri mwezi Julai, 2009. Maandalizi ya Miswada ya Sheria yanakamilishwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Miswada hiyo inatarajiwa kusomwa mara ya kwanza kwenye Bunge la mwezi Aprili 2010.

(iv) **Sheria nyingine na Kanuni zinazoandaliwa**

Wizara kwa kushirikiana na wadau imekamilisha rasimu za mapendekezo ya kutunga sheria mbili (**2)** ambazo ni:

- Sheria ya kuanzishwa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo *(The National Livestock Research Institute Act)*;
- Sheria ya kuanzishwa Maabara Kuu ya Mifugo *(The Central Veterinary Laboratory Act)*.

Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kuandaa na kufanya mapitio ya sheria zifuatazo:-

(i) Rasimu ya awali ya Sheria ya Uzalishajii wa Mbari Bora ya Wanyama (Animal Breeding Act) ya mwaka 2009 imekamilika na itajadiliwa na wadau.
(ii) Rasimu ya kwanza ya mapitio ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (*Marine Parks and Reserves Authority Act*) Na. 29 ya mwaka 1994 imekamilika na itajadiliwa na wadau hivi karibuni.
(iii) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (Tanzania Fisheries Research Institute Act) Na. 6 ya mwaka 1980.imefanyiwa mapitio na rasimu ya kwanza imeandaliwa na itajadiliwa na wadau hivi karibuni.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ya Serikali ya *Mapinduzi* ya Zanzibar imekamilisha kuandaa Kanuni za kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority Act)* Na. 6 ya mwaka 2007 na kuanza kutumika kwa kupewa GN. 48 ya 2009. Kanuni nyingine zilizoandaliwa ni pamoja na:-

- Kanuni **8** zimeandaliwa chini ya Sheria ya Veterinari Na. 16 ya mwaka 2003 (3) na Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya mwaka 2003 (5).
- Kanuni za Uvuvi Fisheries Regulations, 2009 zilikamilishwa kwa GN. 308 ya 2009.
- Rasimu ya Kanuni **6** za Sheria ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008 zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
- Rasimu ya Kanuni 4 za Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008 zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
- Rasimu ya Kanuni za Utotoaji Vifaranga (Hatcheries Regulations) na Uhimilishaji (Artificial Insemination) zimeandaliwa chini ya sheria ya

Magonjwa ya Mifugo na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

- Rasimu ya Kanuni 6 chini ya Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 na Kanuni 2 chini ya Sheria ya Maziwa Na. 8 ya mwaka 2004 zimeandaliwa katika ngazi ya Wizara. Rasimu hizi zitawasilishwa kwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwezi Februari, 2010.

3.3.2 Maendeleo ya Rasilimali Watu

(i) Maendeleo ya Watumishi

Wizara kwa sasa ina jumla ya watumishi **1,869** wa kada mbalimbali. Jumla ya watumishi **771** wamepandishwa vyeo. Aidha, jumla ya watumishi **648** wameajiriwa katika kipindi hicho.

(ii) Masuala ya Jinsia

Wizara imeimarisha dawati la jinsia kwa kulipatia vitendea kazi. Kamati ya Jinsia ya Wizara imeundwa na kupatiwa mafunzo ili kuboresha utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile, viashiria vitakavyotumika katika kufuatilia na kupima mafanikio ya jinsia ndani ya Wizara vimepitiwa na kuboreshwa.

(iii) Vita Dhidi ya Rushwa

Wizara iliendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa katika maeneo ya ununuzi, ajira na utoaji huduma. Katika juhudi hizo Wizara ilizingatia Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2004. Aidha, Ajira ilifanyika kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa 2004 na nafasi za kazi zilitangazwa na kujazwa kwa ushindani ulio wazi kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002.

(iv) Mapambano Dhidi ya UKIMWI

Wizara imeendelea kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) katika kupunguza kuenea kwa UKIMWI kwa kutoa mafunzo kwa watumishi na kununua na kusambaza "condoms" katika ofisi na sehemu mbalimbali. Aidha, Wizara iliendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari kupitia vikao vya wafanyakazi wote, Baraza la Wafanyakazi na mafunzo maalum. Vilevile, Wizara imetoa posho ya lishe kwa watumishi **3** wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa mujibu wa Waraka wa Watumishi wa Umma Na 2. wa mwaka 2006.

(v) Habari, Elimu na Mawasiliano

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kimeimarishwa na Rasimu ya Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara unaandaliwa. Katika kipindi hicho Kitengo kimefanikiwa kutoa nakala **11,000** za jarida la Wizara lenye maelezo kuhusu maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi na nakala **22,000** za kalenda za Wizara ziliandaliwa na kusambazwa. Wizara imeanzisha mtandao wake wenye anuani ya www.mifugo_uvuvi.go.tz na unatumika**.**

4.0 HITIMISHO

Pamoja na mafanikio yaliyoainishwa katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, sekta hizi bado zinakabiliwa na changamoto mbalimbali, ambazo ni pamoja na:

(i) Gharama kubwa za pembejeo za mifugo na uvuvi zikiwemo dawa za kuogeshea mifugo na zana za uvuvi.

(ii) Uhaba wa maeneo ya ufugaji na miundombinu muhimu ya mifugo na uvuvi.

(iii) Uwekezaji mdogo wa sekta binafsi katika sekta ya mifugo na uvuvi.

(iv) Kuwepo kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo na tishio la ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege.

(v) Uhaba wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uhifadhi wa samaki na mazao ya uvuvi.

(vi) Kutokuwepo kwa taasisi za mikopo zenye masharti nafuu kwa wafugaji na wavuvi

(vii) Tija ndogo katika uzalishaji wa mifugo hasa ya asili.

(viii) Kuendelea kuwapo kwa uvunaji na matumizi ya rasilimali za uvuvi yasiyoendelevu, ikiwa ni pamoja na kuibiwa samaki kunakofanywa na meli za kigeni katika Bahari (EEZ).

Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ikishirikiana na wadau wengine wa sekta itaendeleza juhudi zake za kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kuwawezesha wafugaji na wavuvi kuwa na ufugaji bora na uvuvi endelevu utakaoongeza uzalishaji na tija kwa lengo la kuongeza mapato yao na pato la Taifa kwa ujumla.